# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA, MWAKA WA MASOMO 2020/2021

### 1.0 Utangulizi

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na Wadau wote wa Elimu ya juu ndani na nje ya nchi kuwa kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya Kidato cha Sita, Tume imefungua dirisha la kwanza la maombi ya udahili wa Shahada ya Kwanza **kuanzia leo tarehe 26/8/2020** badala ya tarehe 31/8/2020 iliyokuwa imepangwa hapo awali. Dirisha hili litakuwa wazi hadi tarehe 25 Septemba, 2020.

Tume inaendelea kuwahimiza waombaji wote wa udahili kuendelea kupata taarifa rasmi kupitia tovuti ya TCU www.tcu.go.tz , tovuti za vyuo vilivyoruhusiwa kudahili wanafunzi wa Shahada za Kwanza, pamoja na taarifa mbalimbali zinazotolewa na TCU kupitia vyombo vya habari. Vile vile Tume inawahimiza waombaji wa udahili na wananchi kwa ujumla kuhudhuria **Maonesho ya 15 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yatakayofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam ambapo watapata fursa ya kuonana ana kwa ana na Vyuo vya Elimu ya Juu. Maonesho hayo yatafanyika kuanzia tarehe 31 Agosti hadi 5 Septemba, 2020.**

## 2.0 Utaratibu wa Maombi ya Udahili kwa Mwaka wa Masomo 2020/2021

### 2.1 Makundi ya Waombaji wa Udahili

Udahili wa kujiunga na Shahada ya Kwanza utahusu makundi makubwa matatu ya waombaji:

a) Wenye sifa stahiki za Kidato cha Sita;

b) Wenye sifa stahilki za Stashahada (Ordinary Diploma), au sifa linganifu; na

c) Wenye sifa stahiki za "Foundation Programme" ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ili kufahamu sifa stahiki kwa makundi matatu yaliyotajwa hapo juu, waombaji wanaelekezwa kusoma vigezo vilivyooneshwa katika kitabu cha mwongozo cha TCU **(Undergraduate Admission Guidebook for 2020/2021)** kinachopatikana katika tovuti ya TCU www.tcu.go.tz

### 2.2 Utaratibu wa kutuma maombi ya Udahili

a) Maombi yatumwe moja kwa moja kwenye vyuo ambavyo muombaji amevichagua na kuchagua programu za masomo anazozipenda. Mwongozo wa programu zilizoidhinishwa kudahili na vigezo stahiki (**Undergraduate Admission Guidebook for 2020/2021**), unapatikana kwenye tovuti ya TCU www.tcu.go.tz

b) Maelekezo mahsusi ya jinsi ya kutuma maombi yanatolewa na vyuo husika.

### 2.3 Vigezo na Sifa za Waombaji Udahili

Vigezo na sifa katika programu mbalimbali za masomo vinapatikana katika kitabu cha mwongozo cha TCU **(Undergraduate Admission Guidebook for 2020/2021)** katika tovuti ya TCU **www.tcu.go.tz**

### 2.4 Masuala muhimu ya kuzingatiwa na Waombaji

a) Kusoma mwongozo wa udahili uliotolewa na TCU kwa makini na kuelewa kabla ya kuanza kutuma maombi yoyote ya udahili;

b) Kuingia katika tovuti za vyuo ili kujua taratibu za kutuma maombi ya kuomba udahili;

c) Kutuma maombi ya udahili moja kwa moja vyuoni kupitia mifumo ya kielekroniki iliyowekwa na vyuo husika;

d) Kuwasiliana na vyuo moja kwa moja na kupata taarifa za kina kuhusu programu za masomo ili kujiridhisha kabla ya kutuma maombi;

e) **Waombaji wenye vyeti vilivyotolewa nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kuanza kuomba udahili;** na

f) Kuzingatia kalenda ya udahili iliyoidhishwa na Tume **(*Jedwali Na. 1*)** ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

**Jedwali Na.1 Calendar for 2020/2021 Admission Cycle**

| SN | Activity | Responsible | Date |
|---|---|---|---|
| 1. | Publication of 2020/2021 Undergraduate Admission Guidebooks | TCU | 6$^{th}$July 2020 |
| 2. | Beginning of 2020/2021 Admission Cycle | Students and HEIs | 26$^{th}$ August 2020. |
| 3. | Deadline of the first round of applications | Students and HEIs | 25$^{th}$ September 2020 |
| 4. | Deadline of submission of students admitted in the first round | HEIs | 4$^{th}$ October 2020 |
| 5. | Announcement of students admitted in the first round | Students & HEIs | 9$^{th}$ October, 2020 |
| 6. | The Second Round applications | Students & HEIs | 12$^{th}$ – 18$^{th}$ 2020 |
| 7. | Deadline of submission of students admitted in the second round | HEIs | 24$^{TH}$ October 2020 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Announcement of students admitted in the second round of applications | Students & HEIs | 26th October 2020 |
| 9. | Beginning of 2020/2021 Academic year | HEIs | 23rd November 2020 |
| 10. | Transfer window | Students & HEIs | 20th Nov. – 14th Dec. 2020 |
| 11. | Deadline for Submission of transfers | HEIs | 31st December 2020 |
| 12. | Feedback on approved transfers | TCU | 15th January 2021 |
| 13. | The deadline for submission of enrollment data for 2020/2021 Academic year | HEIs | 31st January 2 2021 |

## 3.0 Tahadhari

Wito unatolewa kwa Waombaji wote wa Shahada ya Kwanza endapo wanahitaji kupata ufafanuzi wa suala lolote linalohusu udahili, wawasiliane na vyuo husika moja kwa moja. Wanaweza pia kuwasiliana na TCU wanapohitaji maelezo ya jumla kwa kutumia barua pepe es@tcu.go.tz

***TCU inawaasa wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hapa nchini.***

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
**KATIBU MTENDAJI**
26/8/2020